**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

# TANGAZO LA UFADHILI WA KUJIENDELEZA KWA WATUMISHI WA UMMA KADA ZA AFYA KUPITIA *SAMIA HEALTH SUPER-SPECIALIZATION PROGRAM* KWA MWAKA 2025/2026

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya anawatangazia watumishi wote waliopata udahili wa kusoma masomo ya Shahada ya Uzamili katika fani za afya kwa mwaka 2025/2026 kwamba ufadhili wa ***Samia Health Super Specialization Program 2025*** umefunguliwa. Wizara itaanza kupokea maombi ya ufadhili kuanzia tarehe 20/08/2025 hadi tarehe 12/09/2025. Maombi hayo yatawasilishwa kwa njia ya kielektroniki kwa kutumia 'link' iliyotolewa kwenye tangazo hili. Maombi yatakayofanyiwa kazi ni yale yatakayowasilishwa kwa njia ya mfumo huo tu. Hivyo, waombaji waliowasilisha maombi yao kabla ya tangazo hili wanapaswa kufuata utaratibu huu.

Ufadhili huu ni kwa ajili ya kulipiwa ada ya mafunzo, posho ya kujikimu, nauli pamoja na posho ya utafiti kwa wataalamu watakaopata ufadhili nje ya nchi. Watumishi watakaopata ufadhili kwa vyuo vya ndani ya nchi watalipiwa ada ya mafunzo na posho ya utafiti pindi mtaalamu husika atapokuwa kwenye kipindi cha kufanya utafiti kama sehemu ya mafunzo yake. Malipo ya posho ya utafiti na posho ya kujikimu yatazingatia viwango vilivyopangwa na Wizara.

Vigezo vya ujumla vitakavyotumika kuwapata watakaofadhiliwa ni kama ifuatavyo: -

1. Kuwasilishwa kwa maombi rasmi ya ufadhili kwa njia ya mfumo (Post-graduate Sponsorship Online Application System).

2. Mwombaji awe ni raia wa Tanzania.

3. Awe mtumishi wa Serikali.

4. Awe ana barua ya udahili (admission letter) kutoka kwenye chuo kinachotambuliwa na Serikali ndani au nje ya nchi.

5. Awe anakwenda kusoma masomo ya ubingwa (specialization) au ubingwa bobezi (super-specialization).

6. Taaluma anayoomba kufadhiliwa kwenda kusoma nje ya nchi iwe haipatikani kwenye vyuo vya ndani ya nchi.

7. Mwombaji awe na uzoefu usiopungua miaka mitatu kazini (barua ya ajira na kuthibitishwa kazini iambatishwe wakati wa maombi).

8. Ufadhili utazingatia uhitaji unaotokana na uhaba wa taaluma/fani anayokwenda kusoma mtumishi kwenye kituo husika. Kwa mantiki hiyo, kipaumbele cha kupata ufadhili itategemea upungufu wa taaluma aliyoomba kwenda kusoma kwenye kituo chake cha kazi.

9. Kipaumbele kitatolewa kwa:

    a. Kuzingatia mpango wa mafunzo wa kusomesha wataalamu ulioandaliwa kwa ajili ya kutoa huduma maalum za kibobezi kwenye hospitali za Rufaa za Kanda, Maalum na Taifa.

    b. Wataalamu waliopendekezwa na Taasisi zao kwa ajili ya kusoma mafunzo maalumu ya kimkakati ya ‘seti”.

    c. Watumishi wa Serikali ambao baada ya mafunzo watarudi kwenye vituo vyao vya awali au kupangiwa vituo vingine kulingana na uhitaji.

    d. Waombaji waliodahiliwa katika taaluma za menejimenti na uendeshaji wa huduma za afya kwa mfano, *Health Monitoring and Evaluation, Health Systems Management, Health Policy and Planning, Health Economics, Health Financing, Health Promotion and Health Laws* ambao taaluma hizi zinaendana na kada zao na zitawafanya wapande madaraja.

    *e.* Waombaji waliodahiliwa katika fani ambazo ni za kipaumbele katika utoaji wa huduma za kibingwa.

**<u>Maeneo ya kipaumbele kulingana na hadhi ya kituo cha kutolea huduma.</u>**

**1. Ngazi ya Afya ya Msingi – Baadhi ya taaluma za kibingwa za msingi kama;**

*Obstetric and Gynecology, Pediatrics and Child Health, Internal Medicine, General Surgery.*

**2. Ngazi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa – Taaluma za Kibingwa kulingana na hadhi ya hospitali.**

***Taaluma za Kibingwa Mahsusi***

*Obstetric and Gynecology, Pediatrics and Child Health, Internal Medicine, Emergency Medicine, General Surgery, Orthopedic Surgery, Anaesthesiology, Radiology pamoja na taaluma zote za kibingwa kwenye kada zingine za afya kwenye kituo husika.*

***Taaluma za Kibingwa za ziada***

*Opthalmology, ENT, Oral Health, Urology, Nephrology, Psychiatry, Pathology, Haematology*

**3. Hospitali za Rufaa za Kanda**

***Taaluma za Kibingwa za Msingi kwenye ngazi ya Hospitali za Rufaa za Kanda***

*Obstetric and Gynecology, Pediatrics and Child Health, Internal Medicine, Emergency Medicine, General Surgery, Orthopedic Surgery, Anaesthesiology, Radiology, Opthalmology, ENT, Oral Health, Urology, Nephrology, Psychiatry, Pathology, Haematology, Dermatology, Oncology, pamoja na taaluma zote za kibingwa kwenye kada zingine za afya kwenye kituo husika*

***Taaluma za kibobezi za Msingi kwenye ngazi ya Hospitali ya Rufaa ya Kanda –*** *ni ubobezi (Superspecialization) kwenye maeneo yote ya kibingwa ya msingi kama yalivyoanishwa hapo juu****.***

**4. Hospitali Maalum**

Taaluma zote za kibingwa na kibobezi zinazoendana na aina ya huduma maalum zinatolewa na hospitali husika.

**5. Hospitali ya Taifa**

**-** Taaluma zote za kibingwa kwenye kada za afya hususani zile zenye upungufu kwenye kituo.

-Taaluma zote za kibobezi kwenye utabibu hususani zinazoendana na huduma za kibobezi zinazotolewa hospitalini.

**Vyuo vya Afya ngazi ya kati vya Serikali**

**-**Taaluma zote za kuwajengea uwezo wakufunzi zinazoendana na kada husika ya mkufunzi na zitakazomwezesha kukua na kutambuliwa kwa mujibu wa muundo wa kada yake.

10. Aidha, mwombaji atatakiwa awe ameambatisha nakala halisi za nyaraka zifuatazo wakati wa kufanya maombi: -

   a. Barua ya ruhusa kwenda masomoni kutoka kwa mwajiri wake.
   b. Barua ya udahili kutoka chuoni.
   c. Cheti cha taaluma cha sasa (certificate of highest academic qualification).
   d. Cheti cha usajili na leseni hai kutoka kwenye Baraza la taaluma husika.
   e. Cheti cha kuzaliwa.
   f. Kitambulisho cha Taifa (NIDA).

Maombi yote yawasilishwe kwa kutumia ‘link’ ifuatayo:
https://***esponsorship.moh.go.tz/***

***MUHIMU:*** Kama ilivyoelekezwa hapo juu, maombi yatakayofanyiwa kazi ni yale yatakayowasilishwa kupitia kwenye mfumo tu na mwisho wa kupokea maombi hayo ni tarehe 12/09/2025.

Imetolewa na: -

Katibu Mkuu,
Wizara ya Afya,
Mji wa Serikali Mtumba,
Barabara ya Afya,
S.L.P 743,
**40478 DODOMA.**